# MAJIBU

## NYUMBANI

### A. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi 1**

Vitanzandimi ambavyo vimetungwa viwe vyenye maana na kutumia maneno yenye silabi za sauti zinazokaribiana.

### B. Kusoma

**Zoezi 2**

1. balbu, meza, makochi, televisheni, mapazia, tumbuu, friji, kinu na mchi, mbuzi, sahani, vikombe, sinia, bilauri, jiko la gesi, mafiga, vitanda, neti,
2. sebule, jikoni, msala, hamamuni, vyumba vya kulala
3. Muhtasari ulioandikwa uzingatie ujumbe uliojitokeza kwenye kifungu.

**Zoezi 3**

1. kupiga deki
2. neti
3. tumbuu
4. mafiga
5. kinu na mchi
6. kochi
7. balbu
8. friji

**Zoezi 4**

Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi.

### C. Kuandika

**Zoezi 5**

Insha iwe imezingatia hati nadhifu, urefu unaofaa na kanuni zingine za insha ya wasifu.

### D. Sarufi

**Zoezi 6**

1. mtoto, nyumba, kochi, kitabu, Mombasa, meza, mwalimu, ndugu, mbuzi
2. Sentensi zinazotumia nomino zilizochaguliwa katika nambari ya kwanza ziwe sahihi.

**Zoezi 7**

1. Kupigia mistari vitenzi
   (a) Mtoto <u>anaandika</u> vizuri.
   (b) <u>Nimeenda</u> kucheza na rafiki yangu.
   (c) Mbuzi <u>anakula</u> nyasi.
   (d) Mama <u>ameosha</u> vyombo vyote.
   (e) <u>Usikate</u> miti hiyo, miti ni muhimu.
   (f) <u>Osha</u> matunda kabla ya kuyala.
   (g) <u>Nawa</u> mikono yako unapotoka msalani.
   (h) Daktari <u>amemtibu</u> mtoto mgonjwa.
2. Sentensi zilizotungwa ziwe zimetumia vitenzi vilivyopeanwa na ziwe sahihi.

**Zoezi 8**

1. Kuchagua kivumishi sahihi
   (a) wazuri
   (b) kitamu
   (c) bora
   (d) wema
2. Aya iliyotungwa ihusu nyumbani na itumie vivumishi vinavyofaa.

**Maswali ya Marudio**

1. papa
2. gamba, kamba
3. kuandika mifano ya vitenzi
4. vitenzi
5. vifaa vinavyopatikana nyumbani kama vile kochi, friji, kinu na mchi, balbu, neti, mafiga na kadhalika.
6. Kuunda kitanzandimi chenye maana.
7. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi.
8. Mwanafunzi <u>mzuri</u> amepewa zawadi.
9. ruka, pika, chukua
10. Kuandika insha ya wasifu kuhusu RAFiKI YANGU, insha iwe imezingatia kanuni zifaazo za insha ya wasifu.
11. Kutambua vivumishi katika jedwali: mzuri, hawa, mfupi, yule, jeupe, vile, wazuri, kibaya, mmoja
12. Kuchora

## NIDHAMU MEZANI

### A. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi 1**

1. Kuambatanisha maamkuzi au maagano na majibu
   (a) U mzima – ni mzima
   (b) Alamsiki – binuru
   (c) Makiwa – tunayo
   (d) Siku njema – nawe pia
   (e) U hali gani – njema
   (f) Shikamoo – marahaba
   (g) Umeshindaje – salama
   (h) Salaam aleikum – aleikum salaam
2. Kulinganisha maamkuzi/maagano na wakati wa kutumika
   (a) Alamsiki – usiku
   (b) Makiwa – wakati wa msiba kama vile kifo
   (c) Lala unono – wakati wa kwenda kulala
   (d) Umeamkaje – wakati wa kuamka
   (e) Kwaheri – wakati watu wanapoachana

### B. Kusoma

**Zoezi 2**

Kufuatana kwa maneno katika kamusi
maji, sabuni, shiba, tunda, vitamini

### C. Kuandika

**Zoezi 3**

Kuandika insha za masimulizi kuhusu 'harusi niliyoshuhudia' na 'siku ambayo sitaisahau' insha iwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya masimulizi.

### D. Sarufi

**Zoezi 4**

1. Sentensi zilizotungwa zitumie viwakilishi vilivyopeanwa na ziwe sahihi.
2. Kujaza mapengo kwa kutumia viwakilishi vinavyofaa.
   (a) Sote
   (b) yule
   (c) lenu
   (d) Kwetu
   (e) Hawa

**Zoezi 5**

1. Kupigia vielezi mistari
   (a) Tembea <u>polepole</u> ili usianguke <u>chini</u>.
   (b) Tulitoka <u>nyumbani</u> <u>saa saba</u>.
   (c) Tulicheza <u>sana</u> hadi tukachoka.
   (d) Chakula cha mtoto kilipikwa <u>vizuri</u>.
   (e) Ukila <u>haraka</u> utanyongwa na chakula.
2. Sentensi zilizotungwa zitumie vielezi vilivyopeanwa na ziwe sahihi.

### Maswali ya Marudio

1. Kujaza jedwali la maamkuzi/ maagano na majibu yake.
   (a) Hujambo – sijambo
   (b) Chewa – chewa
   (c) Salaam aleikum – aleikum salaam
   (d) Kwaheri – ya kuonana
   (e) Alamsiki – binuru
   (f) Shikamoo – marahaba
   (g) Umeshindaje – vyema/vizuri/ salama
   (h) Waambaje – sina la kuamba
   (i) Hamjambo – hatujambo
2. shikamoo
3. chakula
4. (a) Mtoto ametembea <u>polepole</u> hadi akafika <u>shuleni</u>.
   (b) Tutaenda <u>sokoni</u> <u>kesho</u>.
   (c) Kimbia <u>haraka</u> ili usichelewe.
   (d) Shangazi huimba <u>vizuri</u>.
   (e) Tutaonana <u>jioni</u>.
5. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na kwa kutumia maneno yaliyopeanwa.
6. Mtoto huyu ni mrefu, <u>yule</u> ni mfupi.
7. Sote
8. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na kwa kutumia maneno yaliyopeanwa.
9. Kamusi ni kitabu cha maneno yaliyopangwa kwa utaratibu fulani na hutolea maneno hayo maana na maelezo mengine.

10. Kuandika insha ya masimulizi kuhusu 'SHEREHE NILIYOIHUDHURIA'. Insha iwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya masimulizi.

## MAVAZI

### A. Kusikiliza na Kuzungumza

#### Zoezi 1

Kulinganisha kitendawili na kiteguzi chake.

(a) Pitia huku nami nipitie kule tupatane pale – mshipi
(b) Bak bandika bak bandua – nyayo
(c) Tega nikutege – mwiba
(d) Daima kidole changu chatokwa na damu kikiangalia chini – kalamu
(e) Hakionekani wala hakishikiki – hewa
(f) Afahamu kuchora lakini hajui akichoracho – konokono
(g) Amefunua jicho jekundu – jua
(h) Aliwa, yuala; ala, yualiwa – papa

### C. Kuandika

#### Zoezi 2

(a) 2,3,4,5
(b)1 – kitengo kikuu cha uchakataji
2 – kiibodi/bodidota
3 – kitufe
4 – kipanya
5 – kiwambo/ skrini
(c) Aya iandikwe kwa kuzingatia maelezo yote yaliyotolewa.

### D. Sarufi

#### Zoezi 3

1. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie viunganishi vilivyopeanwa.
2. (a) kwa sababu
(b) pia
(c) lakini
(d) na
(e) ili

#### Zoezi 4

1. Nguo zimeanikwa juu ya kamba.
2. Nzi ametumbukia ndani ya maziwa.
3. Ng'ombe wetu amefungwa kando ya nyumba.
4. Liweke shati lako chini ya nguo zingine.
5. Gari lilianguka mbali na kanisa.

#### Zoezi 5

1. Kuandika hisia zinazojitokeza kwenye sentensi.
(a) huzuni au majonzi
(b) kukasirika au hasira
(c) mshangao
(d) furaha
(e) shukrani
2. Sentensi zilizotungwa zitumie vihisishi vilivyopeanwa kwa usahihi.

**Maswali ya Marudio**

1. kivuli
2. Chalia, chatembea na chala chakula cha mkono.
3. Mavazi mbalimbali ya wanawake kama vile blauzi, sketi, rinda, buibui na mengineyo.
4. Mchoro uonyeshe umbo kamili la vazi husika.
5. Sentensi iwe sahihi na itumie neno lililopeanwa.
6. kiibodi, vitufe, kipanya, kiwambo/skrini
7. viunganishi
8. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
9. ndani ya, chini ya
10. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.

## DIRA

### A. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi 1**

1. Rejelea kamusi kubaini maana za maneno yaliyopeanwa na mwanafunzi.
2. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.

### B. Kusoma

**Zoezi 2**

1. Faili muhimu ifunguliwe na mazoezi ya kuifunga na kuifungua yafanywe.
2. Kamusi ya mtandaoni itumike kubaini maana za maneno yaliyopeanwa.

### C. Kuandika

**Zoezi 3**

Barua ziandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika barua ya kirafiki.

### D. Sarufi

**Zoezi 4**

1. Tathmini utambulisho wa viambishi.
2. Tathmini majina yalioandikwa.

**Zoezi 5**

1. (a) mtoto – watoto
   (b) simba – simba
   (c) chura – machura/ vyura
   (d) mpishi – wapishi
   (e) kuku – kuku
   (f) papa – papa
   (g) bata – mabata
   (h) nyangumi – nyangumi
   (i) kunguni – kunguni
   (j) kiroboto - viroboto
2. mbu, daktari, kondoo, kobe, mchezaji
3. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.

**Maswali ya Marudio**

1. Maneno yaliyoandikwa yawe yanayoonyesha heshima na adabu.
2. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
3. msalani
4. Mchoro wa dira uonyeshe kaskazini, kusini, mashariki na magharibi.
5. moja (1)
6. Nomino zilizoandikwa ziwe tano (5) na sahihi.
7. chura, kipofu, mitume, madaktari, malenga, mtume
8. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
9. (a) Wapishi wamepika vyakula.
   Mpishi amepika chakula.
   (b) Ng'ombe wamefungwa.
   Ng'ombe amefungwa.
   (c) Mitume waliumia mikono.
   Mtume aliumia mkono.
   (d) Wakunga wamepewa zawadi.
   Mkunga atapewa zawadi.
   (e) Maseremala wametengeneza meza.
   Seremala ametengeneza meza.
10. Barua iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika barua ya kirafiki.

## USHAURI-NASAHA

### A. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi 1**

1. Kueleza maana za methali, kamusi ya methali inaweza ikatumika kutoa maelezo hayo.
2. Kifungu kilichotungwa kitumie methali tatu za malezi.

## B. Kusoma

### Zoezi 2

(a) tatu (3)
(b) minne (4)
(c) kumi na miwili (12)
(d) Nidhamu usisahau, lazima huo ni utu,
(d) Ujumbe ulioandikwa uwe ule unaojitokeza katika kila ubeti.
(e) tarbia

## C. Kuandika

### Zoezi 3

Insha ziandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya maelezo.

## D. Sarufi

### Zoezi 4

1. Tathmini viambishi vilivyotambuliwa
2. Tathmini majina yaliyoandikwa

### Zoezi 5

1. mlima, mpapai, mpira, mwaka, mwezi, muhogo
2. mfereji – mifereji
   mkono – mikono
   mshipi – mishipi
   mguu – miguu
   mkoba – mikoba
   mwembe – miembe
3. Tathmini sentensi zilizotungwa

**Maswali ya Marudio**

1. Tabia za mtoto hulingana na jinsi ambavyo alikuzwa na wazazi au walezi wake.
2. (a) Heshima si utumwa.
   (b) Samaki mkunje angali mbichi.
   (c) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
   (d) Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
   (e) Usipoziba ufa utajenga ukuta.
3. tarbia
4. malenga
5. Shairi lisomwe na ujumbe kuandikwa.
6. Ngeli ya U – I
7. (a) Mgomba umepandwa – Migomba imepandwa.
   (b) Mkeka umenunuliwa – Mikeka imenunuliwa.
   (c) Mlima una theluji – Milima ina theluji.
   (d) Mkate uliliwa – Mikate ililiwa.
   (e) Mkono ule utaoshwa – Mikono ile itaoshwa.
   (f) Mwaka umeisha – Miaka imeisha.
8. (a) Miembe ilizaa sana – Mwembe ulizaa sana.
   (b) Mihogo itapikwa – Mhogo utapikwa.
   (c) Miezi hii ina furaha – Mwezi huu una furaha.
   (d) Mihula iliyopita ilikuwa mizuri – Mhula uliopita ulikuwa mzuri.
   (e) Miavuli ile ni mipya – Mwavuli ule ni mpya.
9. <u>Mchelea mwana</u> kulia hulia mwenyewe.
10. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya maelezo.

# BENDERA YA TAIFA

## A. Kusikiliza na Kuzungumza

### Zoezi 1

Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.

## B. Kusoma

### Zoezi 2

1. Makala mbalimbali yachaguliwe na kusomwa kutoka kwenye vitabu, magazeti au blogi.
2. Kamusi itumike kupata maana ya msamiati uliopatikana katika makala.

## C. Kuandika

**Zoezi 3**

Insha ziandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya wasifu.

## D. Sarufi

**Zoezi 4**

1. (a) jani - majani
   (b) umbo - maumbo
   (c) jino - meno
   (d) shati - mashati
   (e) rinda - marinda
   (f) tunda - matunda
   (g) embe - maembe
2. jiwe, chungwa, yai, neno, rinda
3. Tathmini sentensi

**Zoezi 5**

(a) Jicho limepona – Macho yamepona.
(b) Swali gumu limejibiwa – Maswali magumu yamejibiwa.
(c) Wazo lako litanisaidia – Mawazo yenu yatatusaidia.
(d) Rinda la mtoto litafuliwa – Marinda ya watoto yatafuliwa.
(e) Chungwa limeiva – Machungwa yameiva.

**Maswali ya Marudio**

1. nne (4)
2. maana za rangi ya bendera
   (a) nyekundu – damu
   (b) kijani – mimea
   (c) nyeupe – amani
   (d) nyeusi – rangi ya wakenya
3. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
4. Makala yasomwe na ujumbe kuandikwa kwa ufupi.
5. Nomino za ngeli ya LI-YA ziandikwe kama vile yai, tunda, jino, jicho na nyinginezo.
6. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
7. Jino linauma – Meno yanauma.
8. Macho yatatibiwa na madaktari – Jicho litatibiwa na daktari.
9. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya wasifu.

# MATUNDA NA MIMEA

## A. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi**

1. Kamusi ya nahau itumike kueleza maana za nahau hizo.
2. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie nahau zilizopeanwa.

## B. Kusoma

**Zoezi 2**

Matini yachaguliwe kutoka maktabani na mtandaoni. Matini hayo yasomwe kwa kurejelea mambo ya kuzingatia na mambo ya kuepuka.

## C. Kuandika

**Zoezi 3**

Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya maelezo.

## D. Sarufi

**Zoezi 4**

1. Kuandika wingi wa majina
   (a) kitabu – vitabu
   (b) chombo – vyombo
   (c) kiboko – viboko
   (d) chakula – vyakula
   (e) kitoto – vitoto
2. Kutambua majina ya Ngeli ya Ki-Vi
   kikapu, kiatu, cherehani, kiti, kijumba

**Zoezi 5**

Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.

**Zoezi 6**

joto, jasho, jua, giza, lepe

## Zoezi 7

Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.

**Maswali ya Marudio**

1. Mifano ya nahau za maadili na uraia
2. Maana za nahau, tumia kamusi ya nahau panapofaa.
   (a) Taka radhi – kuomba msamaha
   (b) Piga hodi – bisha ukitaka ruhusa ya kuingia
   (c) Enda msalani – enda haja
   (d) Piga kura – chagua kiongozi
   (e) Kata kesi – fanya uamuzi kuhusu kesi
3. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie nahau zilizopeanwa.
4. Matini isomwe na ujumbe kutambuliwa.
5. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
6. kitambaa, cherehani, kiti, kioo
7. Vyombo <u>vi</u>napendeza.
8. Ngeli ya LI-LI
9. Wingi wa sentensi
   (a) Giza linamtisha mtoto – Giza linawatisha watoto.
   (b) Jasho linatoka sana – Jasho linatoka sana.
   (c) Chaguo lako ni la busara – Chaguo lenu ni la busara.
   (d) Joto limezidi - Joto limezidi.
   (e) Sijapata hata lepe la usingizi - Hatujapata hata lepe la usingizi.
10. Ngeli ya KI-VI
11. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya maelezo.
12. Kuandika umoja wa sentensi
    (a) Vikombe vimeoshwa – Kikombe kimeoshwa.
    (b) Vijibwa vinalala – Kijibwa kinalala.
    (c) Vyoo vile vina vioo vipya – Choo kile kina kioo kipya.
    (d) Viboko vilivunjwa – Kiboko kilivunjwa.
    (e) Vyandarua vilifuliwa – Chandarua kilifuliwa.

# WANYAMA WA PORINI

## A. Kusikiliza na Kuzungumza

### Zoezi 1

1. Kuambatanisha neno na kisawe chake.
   (a) mamba – ngwena
   (b) nyati – mbogo
   (c) barua – waraka
   (d) kifaru – faru
   (e) ndovu – tembo
   (f) kinyonga – lumbwi
2. Kutaja kisawe cha nomino
   (a) ndege – nyuni
   (b) bikizee – ajuza
   (c) nyati – mbogo
   (d) televisheni – runinga
   (e) chakula – mlo
   (f) kilimo – zaraa
   (g) ndovu – tembo
   (h) afya – siha, rai

## B. Kusoma

### Zoezi 2

1. Kujibu maswali ya ufahamu
   (a) Barasa, Imani, Nuru, Baraka
   (b) Mfano wa maelekezo yaliyotumika ni, **(wanafunzi wanne wanacheza uwanjani. Mmoja anajishika kiuno na kusimama mbele ya wenzake.)**
   (c) Maelezo sahihi kuhusu ujumbe uliojitokeza yatolewe. (wanyama wote wa porini ni muhimu)
   (d) Manufaa ya wanyama wa porini ni kuwa ni rasilimali ya nchi na huvutia watalii.
2. Kueleza maana ya mchezo wa kuigiza, maelezo yatolewe kulingana na uelewa wa mwanafunzi.

## C. Kuandika

### Zoezi 3

Insha ziandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya masimulizi.

## D. Sarufi

### Zoezi 4

1. Kusoma sentensi, sentensi zisomwe vizuri na maneno kutamkwa ipasavyo.
2. Kutambua vitenzi na kuviandika daftarini.
   (a) Twiga anakula majani.
   (b) Sisi tunapenda nchi yetu.
   (c) Watoto wanapanda miti.
   (d) Mzee ameketi kwenye kiti.
   (e) Amina anasoma kitabu.

### Zoezi 5

1. Kujaza mapengo
   (a) Nilimpelekea
   (b) alikimbilia
   (c) Aliniandikia
   (d) alimfulia
   (e) amembebea
2. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie nahau zilizopeanwa.

### Zoezi 6

1. Chakula kilipikwa na mpishi.
2. Mama alikata nyama.
3. Gazeti linasomwa na baba.
4. Wimbo mzuri umeimbwa na Amina.
5. Mwenye duka alimwuzia mtoto kitabu.

**Maswali ya Marudio**

1. Kuandika visawe
   (a) kinyonga – lumbwi
   (b) ndovu – tembo
   (c) nyati – mbogo
   (d) tarakilishi - kompyuta
   (e) moyo - mtima
2. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie visawe vya maneno yaliyopeanwa.
3. anaigiza
4. Mhusika ni mtu anayeiga au kufuatiza maneno ama matendo ya mtu mwingine katika mchezo wa kuigiza.
5. Anwani ya mwandikiwa
6. Mifano sahihi ya vitenzi kama vile cheza, imba, ruka na vinginevyo.
7. Kauli ya kutendea
   (a) soma – somea
   (b) cheza – chezea
8. Kauli ya kutendwa.
   (a) pika – pikwa
   (b) ruka – rukwa
   (c) funga – fungwa
9. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie vitenzi vilivyopeanwa.
10. Kusoma insha mtandaoni.

# AFYA BORA

## A. Kusikiliza na Kuzungumza

### Zoezi 1

(a) Kutazama na kuigiza mazungumzo.
(b) Kusikiliza mazungumzo yaliyorekodiwa.

## B. Kusoma

### Zoezi 2

Kusimulia kuhusu taarifa iliyosomwa.

## C. Kuandika

### Zoezi 3

Insha ziandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya maelezo.

## D. Sarufi

### Zoezi 4

Kuandika vinyume vya nomino.
(a) furaha – huzuni
(b) maskini – tajiri
(c) babu – nyanya/bibi
(d) jogoo – koo
(e) kaka – dada
(f) ajuza – shaibu/buda
(g) joto – baridi

(h) jioni – asubuhi
(i) uhuru – utumwa
(j) mama – baba

**Maswali ya Marudio**

1. Kueleza tofauti kati ya mazungumzo rasmi na mazungumzo yasiyo rasmi, maelezo yatolewe kulingana na uelewa wa mwanafunzi.
2. Mifano ya vitendo vya nidhamu katika mazungumzo kama vile kumpa mwenzako nafasi amalize kuzungumza, kuwaruhusu wenzako wachangie mazungumzo, kutumia lugha ya adabu na heshima…
3. Kusoma mazungumzo na kuandika ujumbe.
4. Kusimulia aliyojifunza.
5. Kuandika matini aliyosoma maktabani na kueleza ujumbe.
6. Kuandika kanuni za kuzingatia katika kuandika insha ya maelezo.
7. Kuandika vinyume vya nomino
   (a) mzee - kijana
   (b) jogoo - koo
   (c) kicheko - kilio
   (d) utajiri - umaskini
   (e) shangazi - ami/amu
   (f) mwanafunzi - mwalimu
8. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie vinyume vya nomino zilizopeanwa.
9. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya maelezo.

## KUKABILIANA NA UHALIFU

### A. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi 1**

(a) mfupi kama nyundo
(b) mrefu kama mlingoti
(c) alikonda kama ng’onda
(d) mwembamba kama sindano
(e) mnene kama nguruwe

### B. Kusoma

**Zoezi 2**

1. Kuandika muhtasari wa habari, mwanafunzi aandike ajumbe ulio katika kifungu kwa ufupi.
2. Kujadiliana majibu ya maswali.
   (a) kutoa habari kuhusu mhalifu yeyote, kushirikiana, polisi kushika doria,kukamata wahalifu na kuwafunga jela, kufanya mkutano, polisi kutochukua hongo, watoto kutowasiliana na watu wasiowajua na hatua nyinginezo.
   (b) Wakazi walishirikana na polisi na kutoa habari zozote za uhalifu kwa polisi.
   (c) Kifungu kinahusu kukabiliana na uhalifu.
3. Kujadiliana na mzazi/mlezi kuhusu usalama mtandaoni na manufaa ya ujuzi wa kidijitali.

### C. Kuandika

**Zoezi 3**

Insha ziandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya masimulizi.

### D. Sarufi

**Zoezi 4**

1. Sentensi zilizotungwa ziwe katika wakati uliopita, na ziwe sahihi.
2. Sentensi zilizotungwa ziwe katika wakati uliopo, na ziwe sahihi.
3. Sentensi zilizotungwa ziwe katika wakati ujao, na ziwe sahihi.

**Maswali ya Marudio**

1. Mifano ya tashbihi za umbo na kimo kama vile **mrefu kama mlingoti, mfupi kama nyundo** na **mwembamba kama sindano.**
2. Kukamilisha tashbihi
   (a) mrefu kama mlingoti
   (b) mfupi kama nyundo
   (c) mwembamba kama sindano
   (d) mnene kama nguruwe
   (e) mweusi kama makaa/kizimwili
3. kusoma makala na kutoa maelezo
4. Sentensi ziwe sahihi na katika wakati uliopo.
5. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na katika wakati ujao.
6. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na katika wakati uliopita.
7. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika insha ya masimulizi.

## MAPATO

### A. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi 1**

1. Kujadili njia mbalimbali za kujipatia mapato.
2. Kuelezana jinsi ya kutumia mapato.
3. Kutafuta mtandaoni umuhimu wa mapato na kuziandika hoja.

### C. Kuandika

**Zoezi 2**

Barua ziandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika barua ya kirafiki.

### D. Sarufi

**Zoezi 3**

**Kukanusha sentensi**

(a) Ninacheza mpira – Sichezi mpira.
(b) Ulikula wali – Hukula wali.
(c) Tutaenda sikoni – Hatutaenda sokoni.
(d) Walinunua maziwa – Hawakununua maziwa.
(e) Sisi tutapanda miti – Sisi hatutapanda miti.
(f) Mtapewa vitabu – Hamtapewa vitabu.
(g) Ataupanda mti – Hataupanda mti.
(h) Wanyama wanakunywa maji – Wanyama hawanywi maji.
(i) Utakula ugali wa mtama – Hutakula ugali wa mtama.
(j) Miti inapaliliwa – Miti haipaliliwi.

**Zoezi 4**

1. Kubadilisha nomino katika ukubwa na udogo.

| Wastani | Ukubwa | Udogo |
|---|---|---|
| (a) mti | jiti | kijiti |
| (b) mke | jike | kijike |
| (c) mbwa | jibwa | kijibwa |
| (d) mto | jito | kijito |
| (e) mtu | jitu | kijitu |

2. kijisu, kijike, kijito, kijiji, kijibwa

**Maswali ya Marudio**

1. Kusimulia hadithi yoyote.
2. Mambo ya kuzingatia wakati wa kutoa simulizi.
3. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
4. Kuandika ukanusho.
   (a) Mimi ninaimba – Mimi siimbi.
   (b) Mgeni alikula – Mgeni hakula.
   (c) Tutapata zawadi zetu – Hatutapata zawadi zetu.
   (d) Nyinyi mlipewa pesa – Nyinyi hamkupewa pesa.
5. Barua iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za kuandika barua ya kirafiki.
6. Ukubwa na udogo wa maneno
   (a) mchwa - jichwa - kijichwa
   (b) mke - jike - kijike
   (c) mti - jiti - kijiti
   (d) mji - jiji - kijiji
   (e) mto - jito - kijito

## MAJIBU YA MAJARIBIO

### JARIBIO LA KWANZA

1. Majina ya vitu vinavyopatikana darasani k.v. kifutio, chaki, ubao, saa, chati na kadhalika.
   Kupigia nomino mistari.
2. Tutaosha <u>darasa</u> letu asubuhi.
3. <u>Mama</u> na <u>baba</u> wameketi karibu na <u>darasa</u>.
4. <u>Chungu</u> cha <u>mboga</u> kimewekwa kwenye <u>mafiga</u>.
5. Kuchora picha na kuzipaka rangi.
6. Kuchagua vitenzi (cheza, ruka, imba, soma, pika)
7. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na kutumia maneno yaliyopeanwa.
8. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na kutumia maneno yaliyopeanwa.
9. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na kutumia maneno yaliyopeanwa.
10. mzuri
11. pika
12. Mpishi
13. Andika
14. haya
15. chandarua
16. hatujambo
17. marahaba
18. aleikum salaam
19. njema, nzuri, salama
20. akheri/sabalkheri
21. mchi
22. kutunga kitanzandimi
23. nomino
24. chandarua/neti
25. mafiga
26. balbu
27. kinu na mchi
28. kochi
29. kitanda
30. yule
31. Hiki
32. Wote
33. yangu
34. wengi
35. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na kutumia maneno yaliyopeanwa.
36. Kutambua vielezi(polepole, haraka, vizuri)
37. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi.
38. Insha iliyoandikwa iwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya wasifu.
39. Majina ya wahusika (Mzee Kazana, Bi. Rehema, Nuru, Zawadi, Fanaka na Almasi)
40. Walipata mapato kutokana na kufanya kazi na biashara
41. Nuru na Zawadi
42. chakula – KI-VI
    siku – I-ZI
    mzee – A-WA
43. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na kutumia maneno yaliyopeanwa.
44. Ili waliolala kitandani wasiumwe na mbu
45. Rejelea kamusi kubaini maana za maneno hayo.
46. Kutwanga ama kuponda nafaka/vitu mbalimbali.
47. Mambo yanayoonyesha nidhamu mezani k.v. kula bila kuongea, kufunika kinywa, kupakua chakula anachoweza kumaliza na kadhalika.
48. kupanda miti, kuokota takataka, kutupa takataka katika jalala na kuosha vyombo
49. huongeza vitamin na kusaidia kuimarisha afya
50. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya masimulizi.

### JARIBIO LA PILI

1. sindano
2. macho
3. mwavuli
4. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi.
5. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi.
6. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi.
7. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi.
8. Sabalheri – asubuhi
   Chewa – asubuhi
   Masalheri – jioni
9. Maneno yasomwe vizuri.
10. Methali yoyote inayohusu malezi
11. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kiunganishi kilichopeanwa.
12. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kiunganishi kilichopeanwa.
13. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kiunganishi kilichopeanwa.
14. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kiunganishi kilichopeanwa.
15. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kiunganishi kilichopeanwa.

16. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kihusishi kilichopeanwa.
17. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kihusishi kilichopeanwa.
18. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kihusishi kilichopeanwa.
19. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kihusishi kilichopeanwa.
20. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie kihusishi kilichopeanwa.
21. vihisishi
22. vihusishi
23. mtoto, kipepeo, kuku/jogoo, samaki, twiga
24. mtoto – watoto
    kipepeo – vipepeo
    kuku – kuku
    samaki – samaki
    twiga – twiga
25. kuku, ng'ombe, mwalimu, kipepeo, papa,
26. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie nomino iliyopeanwa.
27. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie nomino iliyopeanwa.
28. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie nomino iliyopeanwa.
29. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie nomino iliyopeanwa.
30. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie nomino iliyopeanwa.
31. Mtoto anakula – Watoto wanakula.
32. Mbuzi amekunywa maji – Mbuzi wamekunywa maji.
33. Mende amekufa – Mende wamekufa.
34. Samaki ana faida – Samaki wana faida.
35. Kuku alitaga yai – Kuku walitaga mayai.
36. Mchoro wa kaptura.
37. Mchoro wa chupi.
38. Mchoro wa rinda.
39. Mchoro wa suruali.
40. Mchoro wa soksi.
41. Mchoro wa dira ambao unaonyesha kusini, kaskazini, mashariki, magharibi
42. Mchoro wa tarakilishi unaoonyesha sehemu zinazohitajika.
43. Aya iandikwe kwa kuzingatia kanuni zilizopeanwa.
44. Kusakura na kusoma matini.
45. Kuandika muhtasari wa makala ya mtandaoni.
46. Hatua za kiusalama mtandaoni
47. Rejelea kamusi kubaini maana za maneno yaliyotajwa.
48. moja
49. Barua ya kirafiki huandikwa na marafiki au jamaa.
50. Barua ya kirafiki iandikwe kwa kuzingatia kanuni za barua ya kirafiki kisha isambazwe mtandaoni.

## JARIBIO LA TATU

1. Methali mbili za malezi
2. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
3. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.
4. Maana ya rangi za bendera zilizotajwa.
5. nyekundu
   nyeupe
6. mshororo
7. Nahau yoyote ya maadili
8. Nahau yoyote ya uraia
9. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie nahau zilizopeanwa.
10. kinyonga – lumbwi
    televisheni – runinga
    ndovu – tembo
11. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie visawe vya maneno yaliyopeanwa.
12. visawe
13. Ngeli ya U – I
14. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
15. Mkoba umewekwa karibu na mti – Mikoba imewekwa karibu na miti.
16. Michezo ya watoto inapendeza – Mchezo wa watoto unapendeza.
17. Mwaka huu una shughuli nyingi.
18. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya maelezo.
19. msumeno, mwaka, migomba
20. ubeti
21. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya wasifu.
22. shati - mashati, embe - maembe, jino - meno, jiko - majiko
23. Ngeli ya U – I

24. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno husika.
25. Wingi wa sentensi zilizotungwa katika nambari ya ishirini na nne.
26. Magari yamenunuliwa.
27. Sikio limeoshwa.
28. Ngeli ya KI – VI
29. Chombo kipya ni cha mjomba.
30. Vyumba vizuri vimejengwa.
31. Kioo cha mama kimewekwa vizuri.
32. Chakula cha mtoto ni kitamu.
33. Chanda chema kimevikwa pete.
34. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
35. Wingi wa sentensi zilizotungwa katika nambari ya thelathini na nne.
36. Ngeli ya LI – LI
37. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
38. Wingi wa sentensi zilizotungwa katika nambari ya thelathini na saba.
39. Mifano ya vitenzi katika kauli ya kutenda.
40. Mifano ya vitenzi katika kauli ya kutendea.
41. Mifano ya vitenzi katika kauli ya kutendwa.
42. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
43. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
44. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
45. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya maelezo.
46. Mamboleo
47. shambani au katika shamba
48. miembe, michungwa, miparachichi, mitufaha
49. maembe na machungwa
50. Babu alikuwa akipalilia mimea.

## JARIBIO LA NNE

| | |
|---|---|
| 1. moja | 2. msalani |
| 3. kwa | 4. langu |
| 5. jeupe | 6. akiponda |
| 7. kinu | 8. kiamshakinywa |
| 9. ndani ya | 10. sote |
| 11. hamjambo | 12. sote |
| 13. huyo | 14. Alitufundisha |
| 15. lo! | 16. mbili (2) |

17. minane (8)
18. Huwa ni furaha yetu, kukuona ukipanda,
19. Shairi linahusu bendera yetu.
20. Nyeusi ni rangi ya ngozi ya Wakenya.
21. Kijani ama kijanikibichi
22. Rangi ya kijani inawakilisha mimea kwenye ardhi yetu.
23. Bendera ni yetu Kenya, Kenya yetu ni bendera,
24. tarbia
25. malenga
26. Kinyume ni neno linalokinzana na jingine.
27. baba – mama
    jogoo – koo
28. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie kinyume cha maneno yaliyopeanwa.
29. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya maelezo.
30. Mifano ya mazungumzo ambayo si rasmi.
31. mrefu kama mlingoti
    mfupi kama nyundo
32. mnene kama nguruwe
    mwembamba kama sindano
33. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie tashbihi zilizopeanwa.
34. Tashbihi ni kulinganisha au kufananisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno k.v. kama, mathalani, mithili ya
35. Insha iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za insha ya masimulizi.
36. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie wakati uliopita.
37. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie wakati uliopo.
38. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie wakati ujao.

39. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie wakati ujao hali ya kuendelea.
40. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie wakati uliopo hali ya kuendelea.
41. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie wakati uliopita hali ya kuendelea.
42. Njia mbili za kujipatia mapato
43. Njia mbili za kutumia mapato
44. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
45. Barua iandikwe kwa hati nadhifu na kwa kuzingatia kanuni za barua ya kirafiki.
46. Wewe hukucheza mpira.
47. Mimi sitakula wali.
48. Yeye hapendi kulala.
49. Sisi hatukutazama mpira.
50. mti – jiti – kijiti
    mji – jiji – kijiji
    mtu – jitu – kijitu

## JARIBIO LA TANO

1. nyanya
2. chezwa
3. marinda
4. mwaka
5. sili
6. sijambo
7. saa
8. dira
9. tembo
10. sindano
11. alikuwa
12. wake
13. huyo
14. lakini
15. kuugua
16. wa
17. ng'onda
18. msamaha
19. walimsamehe
20. asiyesikia la mkuu huvunjika guu
21. kijana
22. Anashauriwa kujiepusha na maovu, pombe, mtandao na kiburi.
23. Maelezo sahihi yakubalike kama vile 'ujana huisha haraka'.
24. Minane (8)
25. Kuwa na tabia nzuri, ujana wako ni moshi
26. Mifano ya tabia nzuri, si lazima mifano hiyo itoke katika shairi.
27. Rejelea kamusi kueleza maana za maneno yaliyopeanwa.
28. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
29. Ushauri unahusu kujiepusha na pombe na kuwachunguza marafiki.
30. Ujumbe wowote sahihi ukubalike.
31. Uwanjani Pambazuka
32. Kuwakumbuka walioshirikiana kupigania uhuru wetu.
33. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu na siku njema huonekana asubuhi.
34. Kueleza maana ya umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.
35. mashariki
36. Rejelea kamusi kueleza maana za maneno yaliyopeanwa.
37. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopeanwa.
38. Kupanda miti na kudumisha usafi wa mwili na mazingira
39. Kuoga, kupiga meno mswaki, kukata kucha, kunyoa nywele na kadhalika.
40. Mashujaa hao walipigania uhuru wa taifa letu.
41. Mifano miwili ya nomino
42. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie vitenzi vilivyopeanwa.
43. yule, kizuri
44. hiki
45. Mifano ya vihusishi k.v. ndani ya, juu ya, mbele ya n.k.
46. Sentensi zilizotungwa ziwe sahihi na zitumie vihisishi vilivyopeanwa.
47. vielezi
48. Sentensi iliyotungwa iwe sahihi na itumie neno lililopeanwa.
49. Ngeli ya LI – YA
50. Mifano ya viunganishi k.v. na, lakini, wala, kwa sababu n.k.